

125

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

**MKATABA WA KUKODISHA GARI-SEMI TRAILER KWA AJILI YA KUSAFIRISHA VIFAA
VYA UJENZI-POLY PIPES, PURLINS, NONDO ZA ZEGE MASHIMO YA MAJI TAKA
KUTOKA KIWARDANI-DAR ES SALAAM KWENDA UTETE RUFUJI**

KWA AJILI YA UJENZI WA CHUO CHA VETA RUFUJI

MKATABA NA: PA/24/2021/2022/TRA/RUF-09

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 08 mwezi 03 - 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha **PWANI, S.L.P. 30345, KIBAHA, PWANI** ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

M/S PASCHAL & SONS TRANSPORT COMMUSION AGENT wa S. L. P.70981 DAR ES SALAAM. (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mzabuni wa usafirishaji vifaa ") kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFUJI;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFUJI;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Mzabuni wa usafirishaji vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kazi za ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya RUFUJI ambayo ujenzi wake unaendelea;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA ZA USAFIRISHAJI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania **2,300,000/=** kwa kuasafirisha vifaa vya ujenzi kutoka Dar es Salaam mpaka eneo la ujezi Utete Rufiji kama

inavyoonekana kwenye jedwari hapo chini kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama “Gharama za usafirishaji vifaa vya ujenzi”

Gharama za kazi zitakazofanyika katika kila jengo ni kama ifuatavyo:

S/N	STAGE	BEI ILIYOKUBALIKA
1	GHARAMA ZITAKAZOTUMIKA KUSAFIRISHA VIFAA VYA UJENZI-POLY PIPES, Z PURLINS, NONDO ZA ZEGE MASHIMO YA MAJI TAKA KUTOKA KIWARDANI KAMAKA KWENDA DAR ES SALAAM MPAKA ENEO LA UJENZI UTETE	2,300,000
	JUMLA	2,300,000

2. MABADILIKO YA GHARAMA ZA USAFIRISHAJI (TRANSPORTATION SUM ADJUSTMENT)

Gharama za usafirishaji hazitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko yoyote yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Malipo yatafanyika baada ya kazi kukamilika yaani Mzigo kufika eneo la ujenzi ukiwa salama na kwa idadi na kiwango kilichotakiwa.

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUHIRISHA KAZI

(a) Mzabuni wa usafirishaji atakabidhi mzigo kwa wahusika wakuu waliopo eneo la ujenzi na kusainisha hati za mapokezi na nyaraka zingine muhimu kuonesha uhalali wa mapokezi ya mzigo husika.

(b) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Mzabuni wa usafirishaji kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo pasipo kuathiri pande zote.

5. WAJIBU WA MZABUNI WA USAFIRISHAJI

Mzabuni atakuwa na wajibu ufuatao: -

Mgogoro wowote utakaotokana na utekelezwaji wa Mkataba huu au baada ya utekelezwaji wa Mkataba utasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote za Mkataba. Iwapo majadiliano yatashindwa kusuluhisha mgogoro, basi upande wowote utatoa Notisi ya siku kumi na nne ya kuupeleka mgogoro usuluhishi kwa njia ya usuluhishi(arbitration).

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA PWANI (PWANI RVTSC)

Jina: CLARA KIBODYA Saini:



Wadhifa: KAMU MKUU WA CHUO Tarehe:

08/03/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: LUKA C. MKIM Saini:




Wadhifa: M/KITII KAMATI YA
REJENZI Tarehe:

08/03/2022

IMESAINIWA NA MZABUNI WA USAFIRISHAJI

Jina: PASCAL PAWA Mbele ya Saini:



Wadhifa: DIRECTOR Tarehe:

8-3-2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: JULIUS TOMBA Saini:



Wadhifa: DIRECTOR Tarehe:

8-3-22